

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE



Simu: 028-2227148
Fax: 028-2227140
E-mail ded.karagwe@kagera.go.tz
ded@karagwedc.go.tz

S. L. P. 20,
KARAGWE

Kumb.Na.KGR/HWK/T.10/1/VOL.XVI/111

23/03/2018

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kuitia Kibali cha Ajira kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Utumishi chenye Kumb. Na. CFC.26/205/01/"FF"/91 kilichotolewa tarehe 22 Agosti, 2017 anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kuajiriwa katika kada ya Mtendaji wa Kijiji III:-

1. Mtendaji wa Kijiji III (Village Executive) Nafasi išhirini na sita (26)

A. SIFA ZA WAOMBAJI

- Waombaji wawe na Elimu ya Kidato cha Nne au cha sita na mafunzo ya Astashahada au cheti katika moja ya fani zifutazo:-
 - Utawala
 - Sheria
 - Elimu ya Jamii
 - Usimamizi wa Fedha
 - Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali .

B. KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJINI III

- Kuratibu na kusimamia upangaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao
- Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Kijiji
- Kusimamia, kukusanya kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Viji
- Katibu wa Mikutano ya Halmashauri ya Kijiji
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Viji
- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi

C. MSHAHARA

- Ngazi ya mshahara itaanza **TGS B** yaani Tshs. 390,000/= kwa mwezi.

D. MASHARTI YA KUAJIRIWA

- Waombaji wanatakiwa kuwa raia wa Tanzania na wawe tayari kufanya kazi sehemu yoyote na wakati wowote.
- Waombaji wawe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji wawe hawajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma.
- Waombaji waambatishe maelezo yao binafsi (CV)
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vyta taaluma, vyeti vyta kidato cha nne (IV) au sita (VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili (2) za rangi za hivi karibuni na ziandikwe majina nyuma.
- Transcript, Testmonial na Provisional Results havitapokelewa wala kukubaliwa
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika TCU na NACTE na taarifa ya uhakiki iambatishwe kwenye maombi.
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za Kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Barua zote ziandikwe kwa mkono.
- Mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe 09/04/2018 saa 9.30 Alasiri.

NB: Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P. 20,
KARAGWE.

Tangazo hili limetolewa na:-


Adeodata A. Peter
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE